

# UFANYE HARAKA KUNISAIDIA

By: F.A.Nyundo  
17/10/1980  
Chang'ombe - Dar

(Kwa upole na huzuni)

Ki li o cha ngu u ki ki si ki a u fa nye ha ra ka ku ni sa i di a

na pi ndi shi da zi na po ni ji a u fa nye ha ra ka ku ni sa i di a

2. Ee Mungu wa ngu ndiwe kimbilio,  
Ewe Bwana wangu ndiwe tegemeo,  
Nikitaabika uje kwangu mbio.

3. Usinitupe wewe ndiye kinga,  
Mimi ni kondoo wewe wanichunga,  
Adui zangu zidi kuwapinga,  
Na giza likija nipatie mwanga.

4. Daima wewe ni wangu msaada,  
Bwana usichoke zidi kunilinda,  
Ukiwa nami sitapata shida,  
Kwa uwezo wako mimi nitashinda.

5. Uniepushe na mwovu shetani  
Ili asinitie majaribuni,  
Mimi mnyonge nakutumaini,  
Wewe uwe nami nifike mbinguni.

6. Unitetee katika hukumu,  
Unisaidie kwa mambo magumu,  
Unisikie na unirehemu,  
Unipe neema ziwe za kudumu.

*Copied By: G.M.Kombo*